

SPACE SCOOP

Bringing news from across the Universe to kids all around the world



EU UNIVERSE
AWARENESS

Anga inaweza Kulipuka!



Mashimo meusi yana sifa mbaya kutokana na sifa yake ya kumeza kila kitu ndani yake na kuvipoteza moja kwa moja. Sifa nydingine ambayo hajulikani sana ni kwamba yana uwezo wa kutengeneza milipuko na kutupa vitu kwa nje. Wanaastronomia wameweza kuğundua milipuko ya aina hii miwili ambayo yofe imeweza kuvunja rekodi!

Galaxi nydingi zina mashimo meusi katika viini vyake, ikiwemo galaxi yetu ya Milk Way. Mashimo haya meusi yanaweza kuwa na uzito zaidi ya mara millioni ya ule wa Jua letu, ambao umekandamizwa katika duara dogo. Maada zilizopakiwa katika duara hilo huwa na nguvu kubwa sana ya mvutano, na kuweza kumeza hata mwanga!

Mashimo meusi yanajulikana sana kwa uwezo wake wa kuvuta maada ndani, kama vile maji yanavyoweza kumezwa katika shimo la sinki. Maada hizo hutengeneza umbo la kisahani kulizunguka shimo jeusi kwa kadri linavyozidi kumeza maada. Milipuko hii mara nydingi huonekana kutokea katika viini vya galaxi zinazowaka sana viitwavyo 'quasars'.

Mmoja kati ya milipuko iliyogunduliwa upo mbali sana tena ni karibu kabisa katika na ukingo wa ulimwengu tunaoujua! Wakati milipuko ule mwindingine unaweza kutoka maada ambazo ni sawa na majua 400 kila mwakal! na nishati ya karibu mara 100 ya nishati ya nyota zote zinazopatikana kwenye Milk Way galaxi. Hii si nguvu ya kawaidal!

COOL FACT

Mashimo meusi sio mashimo kama unvyoweza kudhania na ni kinyume cha kitu kuwa kitupu. Kwani mashimo haya yamebeba maada nydingi ndani yake katika eneo dogo la anga huko ulimwenguni. Jaribu kutengeza modeli ya shimo jeusi kwa kutumia muongozo huu wa UNAWE ili kuğundua zaidi kuhusiana na mashimo haya ya ajabu.



More information about EU-UNAWE Space Scoop: www.eu-unawe.org/kids/